



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA Mtwara
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Simu: 023-2333928

Barua pepe: mtwara@mtwaradc.go.tz

S.L.P. 528,

MTWARA.

02/05/2023

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Wilaya Mtwara inawatangazia wananchi wote walio wazawa kutoka Halmashauri ya Wilaya Mtwara wenye sifa kuomba nafasi ya kazi kwa masharti ya mkataba kamaifuatavyo:

1. MHANDISI DARAJA LA II (ENGINEER II)

1.1 MASHARTI YA KAZI: MKATABA

1.2 MUDA WA MKATABA: MWAKA 1

1.3 SIFA ZA MWOMBAJI: Mwenye Shahada ya Uhandisi kutoka Chuo
Kinachotambuliwa na Serikali na mwenye umri wa
Miaka chini ya 45

1.4 MSHAHARA: Kwa kuzingatia ngazi za mshahara ya watumishi wa
Serikali

1.4 MAJUKUMU YA MHANDISI DARAJA LA II

- i. Kutoa ushauri katika kazi za majengo.
- ii. Kufuatilia utekelezaji wa sheria na kanuni za ujenzi, ukaguzi na kuchukua hatua kwa ukiukwaji wa sheria.
- iii. Kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa na takwimu za ujenzi na ukarabati.
- iv. Kusimamia utekelezaji wa makubaliano ya mikataba inayohusisha masuala ya ujenzi.
- v. Kuanda mpango mkakati wa kuboresha huduma ya usanifu wa majengo.
- vi. Kuandaa mipango na mikakati ya kazi ya ukadiriaji ujenzi.

- vii. Kuandaa taarifa ya kila mwezi, robo mwaka na mwaka kuhusu maendeleo ya miradi ya ujenzi ikijumuisha iliyokamilika na inayoendelea.

2.0 MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji waambatishe vyeti vyao vya kuzaliwa.
- ii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailes C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini walau wawili.
- iii. Maombi yote yaambatane na picha 2 (paspoti size) nakala za vyeti vya taaluma, kidato cha IV na VI na taaluma.
- iv. Mwisho wa kutuma maombi haya ni tarehe 17/05/2023 saa 9:30 alasi.
- v. Maombi yatumwe kwenye anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Mtwara,
S.L.P. 528,
MTWARA

Imetolewa na:


Erica E. Yegella
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MTWARA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MTWARA